BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuanza kuwasilisha Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Azidi kutujaalia amani na upendo, busara na hekima, pamoja na kutuzidishia neema zake zote ambazo ni muhimu sana katika maisha yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Mkutano huu wa Tano wa Baraza hili tukufu kwa kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika;** pia, napenda kuwapongeza wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna

mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, Aidha, pongezi za pekee natoa kwa Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza kwa kura nyingi, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie wote hekma na busara katika jukumu lenu la uongozi ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wa chombo hiki.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar pamoja na Taasisi mbali mbali za Serikali ambazo zimeguswa katika Mswada huu kwa ushirikiano wao mkubwa wakati Kamati ilipokuwa ikijadili kwani michango yao imewawezesha Wajumbe kuufahamu na kuweza kuupitisha kwa urahisi kabisa.

**Mheshimiwa Spika;** hatahivyo, sitokuwa mwingi wa fadhila ikiwa sitowashukuru Wanasheria wa Baraza letu ambao wameshiriki katika kuwapa mafunzo Wajumbe wa kamati hii kwa juhudi kubwa na hatimae kufanikisha Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Kwani sote ni wajibu wetu kuweza kuuchangia kwa maslahi ya watu wetu, lakini pia, kwa faida ya wananchi wote wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika,** sina budi kueleza kuwa, Mswada huu ni marekebisho ya baadhi ya vifungu vya Sheria Kumi na Mbili (12) katika sekta tofauti, ambapo vifungu vingi ndani yake vinafanyiwa marekebisho na kuvirudisha katika sheria zao za awali baada ya Serikali kuona ipo haja ya kufanya hivyo. Aidha, hotuba hii itaeleza kwa ufupi sana baadhi tu ya maoni ya marekebisho ya mswada huu kwani maelezo zaidi tayari mmeshapatiwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** katika marekebisho ya Sheria ya Ajira ya Mwaka 2005 ambayo pia inafanyiwa marekebisho Kifungu cha 5 cha mswada huu, Kamati inashauri kurekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa maneno **"si zaidi ya mwaka mmoja kwa wakati"** yaliyopo baina ya neno **"Kamishna"** na **"kwa".** Vile vile, Kamati inashauri kufutwa maneno **"Sheria ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, 2004"** na

kuwekwa badala yake maneno **"Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar."**.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa sheria zinazofanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Namba 2 ya Mwaka 2009 ambapo Serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuifanya sheria hii kuwa bora na yenye kuleta mantiki iliyobora katika mustakbali wa Taasisi hii kubwa ya Elimu hapa nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri katika Kifungu cha 14 kurekebishwa kama ifuatavyo:-

(a) katika kifungu kidogo kipya cha (4), kuongeza maneno **"wa Taasisi"** katika kifungu kidogo cha (2).

(b) katika kifungu kidogo cha (3), kufutwa neno **"ya"** liliopo katika aya ya (a).

(c) katika kifungu kidogo cha (5), kufutwa maneno **"Mkuu na Makamu Mkuu"** yaliopo katika aya ya (a) na kuwekwa badala yake maneno **"Mkuu na Naibu Wakuu wa Taasisi".**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, inashauri kufanywa marekebisho kwa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii za Zanzibar, Nam. 2 ya Mwaka 2005 Sheria ambayo imekuwa ikilalamikiwa sana na watumishi wa umma tokea ilipofanyiwa marekebisho kwa mara ya mwisho mwaka 2016. Hivyo, ni imani ya Kamati yangu kwamba sasa umefika wakati kwa watumishi wetu kunufaika zaidi kupitia mfuko huu baada ya kuanzisha ndani yake fao jipya la **Upotevu wa Ajira** pamoja na **fao jipya la Kuumia Kazini**.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuifanya Sheria hii iwe bora zaidi katika utekelezwaji wake wa kila siku, Kamati inashauri Kifungu cha 54 kurekebishwa kwa kufutwa maneno **"amepoteza ajira kwa kuachishwa kazi au ajira yake imefikia kikomo"** na kuwekwa badala yake maneno **"ajira yake imefikia ukomo au amepoteza ajira".** Pamoja na ushauri huo, Kamati yetu inaipongeza sana Serikali kwa kuleta mapendekezo hayo ya awali.

Aidha, katika kuleta maana sahihi na inayoendana na uhalisia wake kwa sheria hii, Kamati inashauri katika kifungu hiki cha 54 kufutwa aya ya **"(e)"** na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

> **"atathibitisha kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kuwa hana ajira nyengine, kutoka Tume ya Utumishi, Kamisheni ya Kazi ya Zanzibar na kiapo".**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashauri wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na maoni ya Kamati yetu katika Mswada huu kwani Kamati imepata mafunzo ya kutosha kupitia wataalamu wetu wa Baraza lengo la kuiwezesha Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria hizi ili iwe nyenzo muhimu katika kufanikisha majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha Taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** **Naomba Kuwasilisha**.

Ahsante,

.................................

(*Mhe. Machano Othman Said*)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR